
**Na Rais Thomas S. Monson**



# Kuishi Maisha Tele

Katika mwanzo wa mwaka mpya, Niliwapa changamoto Watakatifu wa Siku za Mwisho kote kufanya uchunguzi muhimu wa kibinafsi na mkamilifu kwa kile ninachokiita maisha tele—maisha yaliyojawa na wingi wa mafanikio, wema, na baraka. Kama vile tulivyosoma herufi za ABC katika shule, natoa ABC yangu ili kutusaidia kupokea maisha tele.

## Kuwa na Mtazamo Halisi

*A* katika ABC zangu inamaanisha mtazamo. William James, mwanzilishi Mwamerika mwanasaikolojia na mwanafalsafa, aliandika, "Mapinduzi makuu ya kizazi chetu ni ugunduzi kwamba wanadamu, kwa kubadilisha mtazamo wao wa ndani, wanaweza kubadilisha hali ya nje ya maisha yao."[1]

Mengi sana katika maisha yanategemea mtazamo wetu. Jinsi tunavyochagua kuona mambo na kujibu wengine huleta tofauti zote Kufanya vyema tuwezavyo na kuchagua kuwa na furaha juu ya hali zetu, zozote zile, kunaweza kuleta amani na utoshelevu.

Charles Swindoll—mwandishi, mwalimu, na mchungaji Mkristo—alisema: "Mtazamo, kwangu, ni muhimu sana kuliko . . . yaliyopita, . . . kuliko pesa, kuliko hali zote, kuliko kutofaulu, kuliko kufaulu, kuliko kile watu wengine wanafikiria au wanavyosema au wanavyofanya. Ni muhimu zaidi kuliko umbo, kipaji, au ujuzi. Itajenga au kubomoa kampuni, kanisa, na nyumba. Jambo la ajabu ni kwamba kila siku tuna nafasi ya kuchagua mtazamo ambao tutachukua kwa siku hiyo."[2]

Hatuwezi kuelekeza upepo, ila tunaweza kugeuza tanga. Kwa furaha tele, amani, na utoshelevu, acha tuweze *kuchagua* mtazamo halisi.

## Jiamini wewe Mwenyewe

*B* Ni kwa kujiamini mwenyewe, katika wale walio pamoja nawe, katika kanuni za milele.

Kuwa mwaminifu kwako mwenyewe, kwa wengine, na kwa Baba yako wa Mbinguni. Mmoja ambaye hakuwa mwaminifu kwa Mungu hadi alipokuwa amechelewa sana alikuwa Kadinali Wolsey ambaye, kulingana na Shakespeare, alikaa maisha marefu katika kuwatumikia wafalme watatu na kufurahia utajiri na mamlaka. Hatimaye, aliondolewa mamlaka yake na mali na mfalme aliyekosa subira. Kadinali Wolsey alilia:

*Laiti ningemtumikia Mungu wangu kwa nusu ya ari*
*Nilimtumikia mfalme wangu, Hangeweza katika umri wangu*
*Kaniacha mimi uchi kwa maadui wangu*[3]

Thomas Fuller, muumini wa Kiingereza na mwanahistoria aliyeishi katika karne ya 17, aliandika ukweli huu: “Haamini, kile ambacho hakiishi kulingana na imani yake.”[4]

Usijikane na usiruhusu wengine kukushawishi kwamba wewe una upungufu katika kile unachoweza kufanya. Jiamini wewe mwenyewe halafu uishi ili uweze kufikia ahadi zako.

Unaweza kupata kile unachoamini unaweza. Tazamia na amini na uwe na imani

### Kabiliana na Changamoto kwa Ujasiri

Ujasiri unakuwa maadili ya maana na muhimu inapotambulika sio sana kama hamu ya kufa kiume bali kama azimio la kuishi kwa wema.

Alisema mwandishi Mwamerika wa insha na mshairi Ralph Waldo Emerson: “Chochote ufanyacho, unahitaji ujasiri. Njia yoyote uamuayo kwenda, kila mara kuna mtu atakayekuambia kwamba umekosea. Kila mara kuna ugumu unaotokea ambao unakujaribu uamini kwamba wakosoaji wako ni sahihi. Ili kubuni mpango wa utendaji na kuufuata mpaka mwisho, kunahitaji kiasi cha ujasiri kama ule mwanajeshi anaohitaji. Amani ina ushindi wake, lakini inahitaji wanaume na wanawake wenye ujasiri ili kushinda.”[5]

Kutakuwa na nyakati ambapo utaogopa na kufadhaishwa. Unaweza kuhisi kwamba umeshindwa. Uwezekano wa kupata ushindi unaweza kuonekana kuwa vigumu. Wakati mwingine unaweza kuhisi kama Daudi anayejaribu kupigana na Goliathi Lakini kumbuka—Daudi *alishinda*!

Ujasiri unahitajika ili kufanya msukumo wa kwanza wa lengo apendalo mtu, lakini pia ujasiri mkuu unahitajika wakati mtu anapojikwaa na lazima tena aweke juhudi ya pili ili kufaulu.

Kuwa na azimio la kufanya bidii, uthabiti wa kutenda lengo jema, na ujasiri sio tu wa kupitia changamoto ambazo lazima zije lakini pia kufanya bidii ya pili, ikiwa itahitajika. “Wakati mwingine ujasiri ni sauti kimya katika mwisho wa siku inayosema, ‘Nitajaribu tena kesho.’”[6]

Na tuweze kukumbuka hizi ABC tunapoanza safari yetu kwenye mwaka mpya, tukikuza mtazamo halisi, imani kwamba tunaweza kutimiza malengo na maamuzi yetu, na ujasiri wa kupitia changamoto zozote zinazoweza kuja katika njia yetu. Halafu maisha tele yatakuwa yetu.


**MUHTASARI**

1. William James, katika Lloyd Albert Johnson, comp., *A Toolbox for Humanity: More Than 9000 Years of Thought* (2003), 127.
2. Charles Swindoll, katika Daniel H. Johnston, *Lessons for Living* (2001), 29.
3. William Shakespeare, *King Henry the Eighth,* act 3, scene 2, lines 456–58.
4. Thomas Fuller, katika H. L. Mencken, ed., *A New Dictionary of Quotations* (1942), 96.
5. Ralph Waldo Emerson, in Roy B. Zuck, *The Speaker’s Quote Book* (2009), 113.
6. Mary Anne Radmacher, *Courage Doesn’t Always Roar* (2009).


### KUFUNDISHA KUTOKA KWA UJUMBE HUU

Fikiria kumwalika mwanafamilia ili kushirikisha uzoefu wa kibinafsi wakati ambapo mtazamo halisi, kujiamani kwao wenyewe, au ujasiri ulipowasaidia. Au waalike ili wapate mifano ya kanuni hizi tatu katika maandiko. Pengine unaweza kujitayarisha kufundisha kwa kufikiria kwa maombi kuhusu maandiko na uzoefu wako mwenyewe.

## VIJANA

## Ujasiri wa Kuepuka Dhoruba

**Na Maddison Morley**

Kwenye usiku wangu wa pili wa kambi ya Wasichana, tulikuwa na mvua kubwa na kimbunga. Kata yangu ilikuwa na karibu wasichana 24 waliohudhuria kambi pamoja na viongozi wao wawili, na sote ilibidi tuingie ndani ya moja ya vibanda viwili ili kujikinga. Mvua ilikuwa inanyesha kwa nguvu, na upepo ulikuwa unaendelea kuwa mbaya sana. Ilibidi nijikumbushe kila mara kuhusu maombi ya usalama ambayo rais wetu wa kigingi aliopeana awali. Kata yetu pia ilitoa ombi letu la kikundi katika kibanda chetu, na nilitoa maombi yangu ya kibinafsi.

Wasichana wengi walipatwa na uoga, na ilikuwa rahisi kuona ni kwa nini. Kibanda chetu hakikuwa chenye nguvu, na tulikuwa karibu na mto. Karibu dakika 20 dhoruba ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba ilibidi kigingi kizima kukimbia kutoka kwa vibanda vyao vya kata hadi kwa vibanda vya washauri ambavyo vilikuwa kwenye mwinuko. Rais wangu wa kigingi alitoa ombi lingine, na tukaimba nyimbo, nyimbo za Msingi, na

nyimbo za kambi katika jaribio la kujifariji wenyewe. Ndio, tuliogopa, lakini tulihisi kwamba kila kitu kingekuwa sawa. Nusu saa baadaye hali ilikuwa SAWA kutuwezesha kurudi tena kwenye vibanda vyetu.

Baadaye tuligundua kilichofanyika kwa kimbunga usiku huo. Kiligawanyika na kuwa dhoruba mbili. Moja ilituzunguka kulia na nyingine kushoto. Tuliyokumbana nayo hata haikuwa mbaya zaidi!

Najua kwamba Mungu alisikia maombi yetu usiku huo na kwamba alitulinda dhidi ya dhoruba mbaya. Ni kwa nini kimbunga kigawanyike isipokuwa Mungu atake kigawanyike? Najua kwamba katika dhoruba za maisha, tunaweza kuomba kwa Mungu Baba wa Mbinguni na atasikia na kutujibu, kutupatia ujasiri na ulinzi tunaohitaji ili kufaulu kwa usalama.

## WATOTO

### Kapteni Moroni

Kapteni Moroni alikuwa na ujasiri alivyokuwa akikabiliana na changamoto. Alipenda ukweli, uhuru, na imani. Alijitolea maisha yake kwa kuwasaidia Wanefi kuhifadhi uhuru wao. Unaweza kuwa kama Kapteni Moroni kwa kupitia changamoto zako kwa ujasiri. Pia unaweza kujitengenezea bendera yako ya uhuru kwa kuandika kwenye kijikaratasi mambo ambayo ni muhimu kwako na kwa familia yako.

**Mahali pa Kupata Mengi Zaidi**

**Alma 46:11–27:** Bendera ya uhuru
**Alma 48:11–13:** Sifa za Moroni

© 2012 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Imechapishwa USA Kiingereza kiliidhinishwa: 6/11. Tafsiri iliidhinishwa: 6/11. Tafsiri ya *First Presidency Message, January 2012.* Swahili. 10361 743

# Kutunza na Kuhudumu kupitia Ufunzaji wa Mwalimu Mtembelezi

Imani • Familia • Usaidizi

*Soma kifaa hiki, na kama ifaavyo, ukijadili pamoja na kina dada unaowatembelea. Tumia maswali ili kukusaidia kuwaimarisha dada zako na kuufanya Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama kuwa sehemu hai ya maisha yako mwenyewe.*

"Ufadhili [umaanisha] zaidi sana kuliko hisia ya huruma," alifunza Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza. "Ufadhili huzaliwa na imani katika Bwana Yesu Kristo na ni zao la Upatanisho Wake."[1] Kwa kina dada wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, ufunzaji wa ualimu tembelezi unaweza kuwa ufadhili katika matendo, njia muhimu ya kufanya imani yetu kwa Mwokozi.

Kupitia kwa ufunzaji wa ualimu tembelezi, tunaweza kutoa utunzaji kwa kuwasiliana na kila dada, kushiriki ujumbe wa injili, na kutafuta kujua mahitaji yake na ya familia yake. "Ualimu tembelezi umekuwa kazi ya Bwana tunapoweka mwangwi wetu kwenye watu badala ya takwimu" anaelezea Julie B. Beck, rais mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama. "Kwa kweli, ualimu tembelezi hauwezi kumalizika kamwe. Zaidi ni njia ya maisha badala ya shughuli. Kuhudumu kwa uaminifu kama mwalimu mtembelezi ni ushuhuda wa ufuasi wetu."[2]

Tunapotoa utunzaji wa daima na wa maombi, tunajifunza jinsi ya kuhudumu vyema kwa na kukidhi mahitaji ya kila dada na familia yake. Kuhudumu kunaweza kuchukua maumbile mengi—mengine makubwa na mengine sio makubwa sana. "Mara nyingi vitendo vidogo vya huduma ndio tu kinachohitajika kuinua na kubarikiana: swala kuhusu familia ya mtu, maneno ya upesi ya kutia moyo, pongezi za kweli, kijibarua kidogo cha shukrani, simu ya muda mfupi," alifunza Rais Thomas S. Monson. "Kama tutakuwa waangalifu na macho, na kama tutatenda kulingana ushawishi unaotujia sisi, tunaweza kukamilisha mengi mazuri. . . . Visivyohesabika ni vitendo vya huduma vinavyotolewa na jeshi kubwa la waalimu tembelezi wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama.[3]

### *Kutoka kwa Historia Yetu*

Mnamo 1843, washiriki wa Kanisa katika Nauvoo, Illinois, waligawanyishwa katika kata nne. Julai ya mwaka huo, viongozi wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama waliwateua kamati tembelezi la dada wanne kwa kila kata. Majukumu ya kamati tembelezi yalijumlisha kukadiria mahitaji na kukusanya michango. Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama ulitumia hii michango kwa kusaidia wenye mahitaji.[4]

Ingawaje waalimu watembelezi hawakusanyi michango tena, wanalo jukumu la kukadiri mahitaji —ya kiroho na kimwili—na kushughulika kukimu mahitaji hayo. Eliza R. Snow (1804–87), rais mkuu wa pili wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, alieleza: "Mwalimu . . . anafaa kuwa hasa na Roho wa Bwana sana, anapoingia katika nyumba ili kujua ni roho gani atakutana nayo hapo. . . . Omba mbele za Mungu na Roho Mtakatifu ili upate [Roho] ili kwamba uweze kutosheleza roho ambayo iliopo katika nyumba hio . . . na uweze kuhisi kuzungumza maneno ya amani na faraja, na kama utapata dada anayehisi baridi, mchukue hata kwenye moyo wako kama unavyomfanya mtoto kwenye kifua chako na kumchangamsha."[5]

**MUHTASARI**

1. Henry B. Eyring, "The Enduring Legacy of Relief Society," *Liahona,* Nov. 2009, 124.
2. Julie B. Beck, "Relief Society: A Sacred Work," *Liahona,* Nov. 2009, 114.
3. Thomas S. Monson, "Three Goals to Guide You," *Liahona,* Nov. 2007, 120–21.
4. Ona *Daughters in My Kingdom: The History and Work of Relief Society* (2011), 105.
5. Eliza R. Snow, katika *Daughters in My Kingdom,*108.

### *Kutoka kwa Maandiko*

Yohana 13:15, 34–35; 21:15; Mosia 2:17; Mafundisho na Maagano 81:5; Musa 1:39.

### *Ninaweza Kufanya Nini?*

**1.** Ninafanya nini ili kuwasaidia kina dada zangu kuhisi kwamba mimi ni rafiki aliye na upendo na anawajali?

**2.** Ninaweza vipi kuwatazama na kuwatunza wengine vyema?

Kwa taarifa zaidi, nenda kwenye reliefsociety.lds.org.

© 2012 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Imechapishwa USA Kiingereza kiliidhinishwa: 6/11. Tafsiri iliidhinishwa: 6/11. Tafsiri ya *Visiting Teaching Message, January 2012*. Swahili. 10361 743